



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



*Unapojibu tafadhali taja:*

**KUMB. NA.AC.215/393/240/25**

**Tarehe: 22/10/2024**

## **TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawataarifu watumishi wote kuwa tumepokea mgao wa fedha za kutoa mikopo kwa watumishi wa umma wa Halmashauri fungu 63CC2 kwa ajili ya kununua Magari, Pikipiki na Samani za ndani.

Hivyo mnatakiwa kuwasilisha maombi ya mkopo huu kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

### **MASHARTI KWA UJUMLA**

- i. Mwombaji awe mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anayebakiwa na 1/3 ya mshahara wake baada ya makato ambayo yatarejeshwa ndani ya miezi isiyozidi Miezi 72 yaani isiyozidi miaka 6.
- ii. Mwombaji awe amethibitishwa kazini kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma
- iii. Mkopo huu haununui deni kutoka taasisi nyingine zinazotoa mikopo kwa watumishi wa umma
- iv. Mwombaji asiwe na shauri lolote la kinidhamu au jinai
- v. Mkopo huu haufanyi "top up" ikiwa una mkopo huu unaoendelea hautaruhusiwa kuomba hadi utakapomalizika.
- vi. Aidha, iwango cha mkopo kitategemea na ngazi ya mshahara ya mtumishi husika
- vii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/10/2024 saa 3:30 Asubuhi .

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa Hazina Portal kwa kutumia link ifuatayo [als.muse.go.tz](https://als.muse.go.tz) kwa kufuata hatua zifuatazo;-

1. Ingia katika google, yahoo search tafuta neno Hazina portal au ingia link [als.muse.go.tz](https://als.muse.go.tz)

2. Mfumo utafunguka utaingia kuanza kujisajili kwenye dirisha la Register ambapo utaingiza taarifa zako kama zilivyo katika Salary slip yako ya hivi karibuni.
3. Utathibitisha taarifa zako kwa kutumia email na namba za simu unazozitumia
4. Baada ya kuthibitisha sasa utaingia katika mfumo ambapo utaingia katika dirisha la Advanced loan
5. Ingia Apply loan ingiza kiasi unachotaka kukopa



Husna Toni

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**NYANG'HWALE**



**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**S.L.P 352**  
**NYANG'HWALE**

---

**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Geita,**  
**Barua pepe:ded@nyago.tz Tovuti: [www.nyanghwale.go.tz](http://www.nyanghwale.go.tz)**